

#### 4.0 MUDA WA CHETI CHA USAJILI NA LESENI YA ALAMA YA UBORA

Leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS na Cheti cha usajili wa majengo hudumu kwa mwaka mmoja (1) na huhuishwa baada ya kuhakikisha kwamba taratibu zilizokubalika zinafuatwa.

Cheti cha usajili wa bidhaa hudumu kwa miaka mitano (5).

#### 5.0 GHARAMA KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI

Serikali hutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati pale wanapomba bidhaa zao wanazozilisha wenyewe zithibitishwe ubora. Kati yao wapo ambao wanasamehewa kulipa ada yoyote kwa sababu ya mitaji yao kuwa midogo.

#### Ili kupata msamaha huu, mjasiriamali anatakiwa:

- Kupata barua ya utambulisho kutoka ofisi ya SIDO.
- Kuwa na leseni ya biashara.

Wajasiriamali waliokwisha pata leseni ya kutumia alama ya ubora wanapaswa kutunza taarifa za uzalishaji na mauzo ambazo watatakiwa kuzionesha kwa wakaguzi wa TBS pindi zinapohitajika.

**Kwa maelezo zaidi,wasiliana nasi kwa anwani zifuatazo:**

#### **MKURUGENZI MKUU**

##### **Shirika la Viwango Tanzania (TBS)**

S.L.P. 9524, Dar es Salaam

**Simu:** +255 22 2450298 / 2450206/2451763-6

**Hotline:** +0800 110 827/ **Nukushi:** + 255 22 2450959

**Baruapepe:** info@tbs.go.tz/ **Tovuti:** www.tbs.go.tz

**Malalamiko:** malalamiko@tbs.go.tz

#### **OFISI ZA KANDA:**

##### **NYANDA ZA JUU KUSINI**

Jengo la NHIF, Ghorofa ya 7

S.L.P. 1674 Mbeya, Tanzania

**Simu:** 025 2502848 / **Nukushi:** 025 2502848

##### **KANDA YA ZIWA**

Jengo la NSSF, Ghorofa ya 5

S.L.P. 1814 Mwanza, Tanzania

**Simu:** 028 2505044 / **Nukushi:** 028 2505044

##### **KANDA YA KASKAZINI**

Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2

S.L.P. 2399 Arusha, Tanzania

**Simu:** 027 2520143 / **Nukushi:** 027 2520143

##### **KANDA YA KATI**

Jengo la PSSSF, Dodoma Plaza, Ghorofa ya 6

S.L.P 2956, Dodoma, Tanzania

**Simu:** 026 2320310 / **Nukushi:** 026 2320310

##### **KANDA YA KUSINI**

Jengo la MTUWASA

S.L.P 1396 Mtwara, Tanzania

**Simu:** 023 2334477 / **Nukushi:** 023 2334477

##### **KANDA YA MAGHARIBI**


Jengo la NSSF (Mafao House), Ghorofa ya 2

S.L.P 1276 Kigoma, Tanzania

**Simu:** 028 2804023 / **Nukushi:** 028 2804023



## SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)



**UTARATIBU WA USAJILI  
WA BIDHAA / MAJENGO  
NA KUPATA ALAMA YA  
UBORA**

## 1.0 UTARATIBU WA USAJILI WA BIDHAA

TBS husajili bidhaa za vyakula na vipodozi zinazozalishwa nje ya nchi na kuingizwa nchini. Bidhaa zinazokidhi viwango tu ndizo husajiliwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini.

Maombi ya usajili hufanyika katika **mfumo wa kielektroniki (OAS)** unaopatikana katika tovuti ya TBS ([www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)).

### 1.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Mwombaji hutakiwa kujisajili katika mfumo na kisha kuingiza taarifa za bidhaa anazotaka kusajili.

### 1.2 Hatua ya Pili – Malipo

Mwombaji hupewa gharama za kusajili bidhaa husika pamoja na namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali kupitia kwenye mfumo wa kielektroniki.

Baada ya malipo hutakiwa kuwasilisha sampuli katika ofisi za TBS.

### 1.3 Hatua ya Tatu – Tathimini

Bidhaa hufanyiwa tathimini na mwombaji atapewa mrejesho kupitia mfumo wa kielektroniki (OAS) kama bidhaa imekidhi vigezo au la.

### 1.4 Hatua ya Nne – Usajili

Bidhaa zinazokidhi vigezo husajiliwa na cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa kielektroniki.

## 2.0 UTARATIBU WA USAJILI WA MAJENGO

TBS husajili majengo yanayohusika na biashara za vyakula na vipodozi.

Maombi ya usajili hufanyika katika **mfumo wa kielektroniki (OAS)** unaopatikana katika tovuti ya TBS ([www.tbs.go.tz](http://www.tbs.go.tz)).

### 2.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Mwombaji hutakiwa kujisajili katika mfumo na kisha kuingiza taarifa za jengo analotaka kusajili.

Mwombaji anatakiwa kuambatisha picha ya mchoro wa jengo, leseni ya biashara pamoja na ramani inayoelekeza jengo lilipo ili kuwezesha wakaguzi kulifikia.

### 2.2 Hatua ya Pili – Malipo

Mwombaji hupewa gharama za kulipia kulingana na aina ya shughuli anayofanya katika jengo husika pamoja na namba ya kumbukumbu ya malipo ya serikali kupitia mfumo wa kielektroniki.

### 2.3 Hatua ya Tatu – Tathimini

Baada ya malipo kufanyika Mkaguzi atafika kukagua jengo kulingana na vigezo vilivyowekwa ili kujiridhisha na kisha mwombaji atapewa mrejesho.

### 2.4 Hatua ya Nne – Usajili

Jengo lililokidhi vigezo husajiliwa na cheti cha usajili hutolewa kupitia mfumo wa kielektroniki.

## 3.0 UTARATIBU WA KUPATA ALAMA YA UBORA

Zipo hatua mbalimbali ambazo mzalishaji hupaswa kuzizingatia kabla ya kupata leseni ya kutumia alama ya ubora ya TBS kwenye bidhaa yake.

### 3.1 Hatua ya Kwanza – Maombi

Maombi ya uthibitishaji ubora hufanywa na mwombaji kwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa maandishi.

Majibu hutolewa yakielezea taratibu za kufuata na gharama zote zinazohitajika. Majibu huambatana na fomu maalum ambayo mwombaji hujaza na kuirudisha TBS ikiwa na viambatisho vifuatavyo:

- Mtiririko wa uzalishaji wa bidhaa husika;
- Mfumo wa uongozi ukionyesha kitengo cha udhibiti ubora;
- Orodha ya malighafi anazotumia na mahali zinakotoka kwa kila bidhaa;
- Ramani inayoelekeza jinsi ya kufika kiwandani kwake.

Baada ya kutekeleza na kuwasilisha nyaraka tajwa, tarehe ya kufanya ukaguzi wa awali hupangwa. Izingatiwe kuwa mwenye kiwanda anatakiwa kuwa katika uzalishaji siku ya kufanya ukaguzi wa awali.

### 3.2 Hatua ya Pili – Ukaguzi wa Awali

Ukaguzi wa awali hufanywa na wakaguzi wa TBS. Sampuli huchukuliwa na kupimwa ili kuona kama bidhaa inakidhi matakwa ya kiwango husika. Mkaguzi huandaa taarifa kuhusu hali halisi ya kiwanda na mambo yanayostahili kurekebishwa.

### 3.3 Hatua ya Tatu – Upimaji

Sampuli zilizochukuliwa hupimwa katika maabara za TBS kwa kufuata kiwango husika. Baada ya kazi ya upimaji kumalizika, ripoti hutolewa kwa mwombaji.

### 3.4 Hatua ya Nne – Utoaji wa Leseni

Uamuzi kuhusu kutoa au kutotoa leseni ya kutumia alama ya ubora hutegemea tu ripoti ya ukaguzi wa awali wa kiwanda pamoja na ripoti ya maabara. Kimsingi ripoti zote mbili zinatakiwa kuonyesha kwamba mazingira ya uzalishaji kiwandani, mfumo wa uzalishaji na bidhaa iliyopimwa havina matatizo.

Ikiwa sivyo basi mzalishaji hutakiwa kufanya marekebisho na baadaye mkaguzi wa TBS hutumwa tena na kuleta sampuli nyingine.